*Kioo cha Lugha, Juz. 22(2), 292-309*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v22i2.9

# Michakato ya Kisintaksia ya Uundaji wa Sentensi Changamani za Kiswahili

*Sephania M. Kyungu[1] na Luinasia E. Kombe[2]*

## Ikisiri

Makala hii inalenga kuchambua michakato ya kisintaksia ya uundaji wa sentensi changamani za Kiswahili kwa kubainisha namna kishazi kikuu na kishazi bebwa vinavyowekwa pamoja kuunda sentensi hizo. Ili kufanikisha lengo hilo, makala imeongozwa na Nadharia Rasmi ya Chomsky (1965). Data za makala hii ni sentensi changamani za Kiswahili ambazo zilikusanywa kwa njia ya usomaji wa matini kutoka katika riwaya na magazeti. Matini hizi ziliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji nasibu sahili. Uchambuzi wa data ulifanyika kwa mkabala wa kitaamuli kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimaudhui. Makala hii imebaini kwamba kuna michakato mitatu inayotumika kuunda sentensi changamani ambayo ni uchopekaji, udondoshaji-chopezi na udondoshaji-chopezi hamishi. Kwa kutumia Nadharia Rasmi, imebainika kwamba kila mchakato una hatua zake katika kuunda sentensi changamani.

## 1.0 Utangulizi

Neno 'mchakato' katika makala hii limefasiliwa kama shughuli ya kiisimu inayoweka pamoja vipashio vya kisintaksia ili kuunda tungo fulani yenye maana inayokubalika. Maelezo haya yanashadidiwa na Tallerman (2011) anapoeleza kuwa vipashio vya kisintaksia hujumuishwa pamoja kiulalo au kiusilisila kwa kufuata michakato. Kwa kuzingatia maelezo hayo, tunapoongelea suala la michakato ya kisintaksia ya uundaji wa sentensi changamani, tunamaanisha shughuli za kiisimu zinazofanyika ili kushusha hadhi kishazi kimojawapo kati ya vishazi huru viwili. Hatimaye, kuviunganisha vishazi hivyo, yaani kishazi huru na kile kilichoshushwa hadhi kuwa kishazi tegemezi. Kishazi huru hufasiliwa kwa kujiegemeza kisemantiki zaidi ambapo hufasiliwa kama ni kishazi kinachoweza kutumika peke yake na kuleta maana kamili katika mawasiliano bila kutegemea

[1] Mhadhiri Msaidizi, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: Sephaniakyungu06@gmail.com

[2] Mhadhiri, Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: kombeluinasia@gmail.com

kishazi kingine (Wesana-Chomi, 2017). Kishazi hiki ni kiambajengo kikuu cha sentensi changamani ambacho huambatana na vishazi vingine vilivyoshushwa hadhi na kuwa vishazi tegemezi. Kishazi tegemezi hakiwezi kutumika peke yake na kuleta maana kamili. Hiki ni aina ya kishazi ambacho kimuundo hubebwa ndani ya kishazi kikuu. Hii ni kwa sababu kishazi hiki huwa hakiwezi kutoa maana kamili, hivyo, hulazimika kubebwa ndani ya kishazi kikuu. Kwa hiyo, kimuundo kishazi tegemezi huitwa kishazi bebwa na kishazi huru huitwa kishazi kikuu.

Wesana-Chomi (2017) anaeleza kuwa katika sintaksia ya Kiswahili kuna michakato miwili inayohusika katika uundaji wa sentensi changamani ambayo ni urejeshaji na ujalizaji. Kuhusu mchakato wa urejeshaji, Wesana-Chomi anasema unatokana na dhana ya urejeshi. Anaendelea kueleza kuwa urejeshi huo hutokea katika kitenzi pale tendo fulani linaporejeshwa kwa nomino. Mfano namba 1 unadhihirisha zaidi hoja hii.

1. Kisu *kili**cho**potea* kimepatikana.

**Chanzo:** Wesana-Chomi (2017: 138)

Katika mfano namba 1, kiambishi {-*cho*-} kinarejelea nomino *kisu*. Kiambishi hicho hujulikana kama kiambishi rejeshi. Urejeshaji huu huzalisha tungo rejeshi ambazo zimeelezwa na Mekacha (1987) kama mojawapo ya tungo tegemezi. Mekacha anaeleza kuwa tungo tegemezi ni sentensi iliyoshushwa hadhi na kutegemezwa ndani ya sentensi nyingine. Hii ina maana kwamba tungo tegemezi haitokei peke yake bali hutokea kama kiambajengo cha sentensi kuu. Urejeshaji umeelezwa na Wesana-Chomi (2017) kama moja ya michakato inayotumika kuunda sentensi changamani. Chunguza mfano namba 2 kwa ufafanuzi zaidi.

2. Polisi wamemkamata mfungwa ali**ye**toroka jela jana.

**Chanzo:** Wesana-Chomi (2017: 177)

Wesana-Chomi anaeleza kwamba tungo ya mfano namba 2 ni matokeo ya mchakato wa urejeshaji ambao unaunganisha sentensi ya kwanza (kuanzia sasa $S_1$) na sentensi ya pili (kuanzia sasa $S_2$) kama mfano wa 3 unavyoonesha.

3. [$S_1$Polisi wamemkamata mfungwa] [$S_2$ Mfungwa alitoroka jela jana]

Mekacha (1987) na Wesana-Chomi (2017) wanaelekea kukubaliana kwamba sentensi ya mfano namba 2 imeundwa kwa mchakato wa urejeshaji. Msingi wa madai yao ni kwamba nomino radidi katika $S_1$ na $S_2$ hugeuzwa na kuwa kiambishi rejeshi. Kulingana na mfano huo nomino radidi ni *mfungwa* ambayo imetokea katika $S_1$ na $S_2$ kama mfano namba 3 unavyoonesha. Kwa mujibu wa Wesana-Chomi, nomino hiyo imegeuzwa na kuwa kiambishi rejeshi ambacho katika huo mfano wa namba 2 ni {-ye-}. Hata hivyo, kuhusu nomino radidi kugeuzwa kuwa

kiambishi rejeshi ni suala la mjadala ambalo litajadiliwa kwenye sehemu ya uchambuzi wa data katika makala hii.

Pia, Wesana-Chomi (2017) anaeleza kwamba sentensi changamani za Kiswahili zinaundwa na mchakato wa ujalizaji. Kwa mujibu wa mtaalamu huyu, ujalizaji huunda sentensi hizo kwa vishazi vikuu viwili huku kishazi kimoja kikitanguliwa na viunganishi tegemezi kama vile: *kama*, *kwamba* na *kuwa* katika muundo wa nje. Katika hali kama hiyo, kishazi kikuu kinachotanguliwa na viunganishi tegemezi hushuka hadhi na kuwa kishazi bebwa. Tazama mfano namba 4(a na b) kwa ufafanuzi zaidi.

4. (a) [$S_1$ Julia amepata tetesi] [$S_2$ *kuwa Cheusi ni mke wa Hamisi*]
   (b) [$S_2$ Jumanne ameleta habari] [$S_2$ *kwamba mgonjwa amefariki leo usiku*]

**Chanzo:** Wesana-Chomi (2017: 179)

Katika namba 4(a na b) vishazi bebwa vimeandikwa kwa hatimlazo na kutokea kama viambajengo vya $S_1$. Kishazi bebwa cha katika mfano namba 4(a) kinajaliza nomino *tetesi* ya $S_1$ ilhali kishazi bebwa katika mfano 4(b) kinajaliza nomino *habari* ya $S_1$. Kabla ya sentensi hizo kuwa hivyo katika muundo wa nje, muundo wa ndani ulikuwa kama zinavyooneshwa katika mfano wa 5(a na b).

5. (a) [$S_1$ Julia amepata tetesi] [$S_2$ Cheusi ni mke wa Hamisi]
   (b) [$S_1$ Jumanne ameleta habari] [$S_2$ Mgonjwa amefariki leo usiku]

Wesana-Chomi (*keshatajwa*) anaeleza kuwa katika kuunganisha $S_1$ na $S_2$ kiambajengo $S_2$ hukunjiwa katika muundo wa $S_1$ kama inavyooneshwa katika 4(a na b). Katika muundo kama huo, $S_2$ hufanya kazi kama kijalizo[3] cha nomino. Maelezo haya ya Wesana-Chomi kuhusu ujalizaji yanahusu dhima ya kishazi bebwa na sio mchakato wa kisintaksia. Kuhusu dhana hii kuwa ya kidhima imedokezwa pia na Philipo na Kuyenga (2018) ambao wanaeleza kuwa ujalizaji ni dhana iliyobuniwa na wanasarufi ili kuelezea uhusiano unaojitokeza pale kauli mbili au zaidi zinaposhikamanishwa kuwa kauli moja. Hali ikiwa hivyo, kauli moja hufanya kazi kama kijenzi mahususi cha kauli nyingine. Maelezo haya yanaonesha dhahiri kwamba ujalizaji si mchakato wa uundaji wa sentensi changamani bali ni matokeo ya mchakato wa kisintaksia wa uundaji wa sentensi changamani za Kiswahili. Kwa kuwa ujalizaji si mchakato wa kimuundo bali ni matokeo ya mchakato wa kisintaksia wa uundaji wa sentensi changamani za Kiswahili, makala hii imelenga kuweka bayana michakato inayotumika kuunda hizo sentensi changamani.

---

[3] Kijalizo ni kipashio kinachokamilisha kipashio kingine katika tungo (Philipo na Kuyenga, 2018).

Makala hii ina sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza ni utangulizi. Sehemu ya pili inahusu methodolojia ya utafiti. Sehemu ya tatu imefafanua Nadharia Rasmi ambayo imetumika katika makala hii. Sehemu ya nne imeshughulikia ufafanuzi kuhusu michakato ya uundaji wa sentensi changamani za Kiswahili. Sehemu ya mwisho ni hitimisho linalofuatiwa na orodha ya vifupisho vilivyotumika katika makala hii. Hivyo, baada ya sehemu hii ya utangulizi, sehemu inayofuata inahusu methodolojia ya utafiti.

## 2.0 Methodolojia ya Utafiti

Makala hii imetumia sehemu ya data za utafiti wa Shahada ya Umahiri[4] wa mwandishi mmoja wa makala hii. Data za utafiti huo zilipatikana katika riwaya na magazeti. Uteuzi wa matini hizi ulichochewa na maelezo ya Meyer (1996) na Kortmann (1997) kuwa matini zilizoandikwa ni faafu zaidi katika ufafanuzi wa sarufi kwa kuwa hazikiuki kanuni za kisarufi kama ilivyo matini za mazungumzo. Sampuli ya matini hizo ilichaguliwa kwa mbinu ya usampulishaji nasibu. Kwa kuzingatia mbinu hii, kila riwaya na magazeti rasmi vilikuwa vinafaa kutumika kama chanzo cha data. Kutokana na wingi wake mtafiti asingeweza kutumia riwaya zote na magazeti yote. Hivyo, ili kupata sampuli wakilishi mtafiti alilazimika kutumia mbinu nyingine ya usampulishaji ambayo ni usampulishaji nujumu.

Katika mbinu hii mtafiti huchagua sampuli kutokana na wango lililopo karibu naye linalofikika au kupatikana kirahisi. Kwa kutumia mbinu hii, mtafiti alipata riwaya sita. Baada ya kuona riwaya zote sita zimesheheni sentensi changamani, mtafiti alitumia mbinu ya usampulishaji nasibu sahili ili kupata riwaya mbili. Kwa kutumia mbinu hii, majina sita ya riwaya yalipewa namba ambazo ziliandikwa kwenye vikaratasi. Ili kuepuka upendeleo, mtafiti, alivikunja vikaratasi hivyo, kisha akamuomba mkutubi amsaidie kuchagua vikaratasi viwili. Namba zilizochaguliwa kupitia mbinu hiyo zilihusisha riwaya za *Haramu* (2004) na *Mwendo* (2004).

Vilevile, kwa kutumia mbinu ya usampulishaji nujumu, majina sita ya magazeti rasmi aliyopatiwa mtafiti, aliyapa namba kulingana na alivyopewa. Gazeti lililotajwa la kwanza lilipewa jina na namba na kuendelea hivyo hadi sita. Baada ya kitendo hicho, karatasi hizo zilikunjwa na kuwekwa mezani. Baada ya kufanya hivyo, mtafiti alimuomba rafiki yake achague kikaratasi kimoja tu kati ya sita. Gazeti lililochaguliwa kutokana na mchakato huo ni *Mwananchi* linalochapishwa na *Mwananchi Communications Ltd*. Kwa kuwa gazeti hilo huchapishwa kila siku, usampulishaji nasibu sahili ulitumika tena kupata tarehe moja kati ya tarehe za mwezi Juni mwaka 2021 kwani ndio mwezi ambao mtafiti

[4] Tasinifu ya shahada ya umahiri ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam yenye kichwa: *Uchambuzi wa Michakato ya Kisintaksia katika Uundaji wa Sentensi Changamani za Kiswahili*.

alikuwa anakusanya data. Tarehe za mwezi husika ziliorodheshwa kwenye vikaratasi. Kila tarehe ndani ya mwezi huo iliandikwa kwenye kikaratasi chake, kisha mtafiti alikunja vikaratasi hivyo na kumuomba rafiki yeke aokote kikaratasi kimoja tu kati ya vikaratasi thelathini. Tarehe iliyoandikwa kwenye kikaratasi kilichookotwa ndiyo tarehe ambayo gazeti husika lilisomwa ili kupata data. Tarehe iliyochaguliwa kutokana na mchakato huo ni 26.06.2021.

Mbinu ya usomaji wa matini ilitumika kukusanya data za utafiti huo. Kutokana na usomaji wa matini teule, zilipatikana sentensi changamani ambazo baadaye zilichambuliwa kwa kuchunguza michakato iliyotumika kuziunda. Uchambuzi wa data ulifanyika kwa mkabala wa kitaamuli kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimaudhui.

Kwa kuwa makala hii ni sehemu tu ya utafiti huo wa umahiri, haikuwa rahisi kutumia data zote za utafiti huo katika makala hii. Hivyo, data zilizotumika katika makala hii zimetoka katika riwaya ya *Mwendo* na gazeti la *Mwananchi* pekee.

## 3.0 Nadharia Rasmi

Nadharia Rasmi iliasisiwa na Chomsky mwaka 1965. Madai ya nadharia hii ni kwamba muundo wa ndani ndio unaodhihirisha maana kwa kuteua maneno yenye kubeba maana iliyokusudiwa na kuyapanga kwa namna itakayofikisha maana hiyo. Muundo wa ndani huzalishwa na kitengo cha msingi chenye msamiati, taarifa za upanuzi wa sentensi na dhima za sentensi. Muundo wa ndani hupitia katika kitengo cha mageuzi na kuzalisha muundo wa nje. Kitengo hiki kina mageuzi ya hiari ambayo ni udondoshaji, uhamishaji, uchopekaji na ubadala. Hivyo, muundo wa nje huzalishwa kwa mageuzi hayo. Makala hii imetumia maarifa haya ya Nadharia Rasmi katika kuchambua michakato ya kisintaksia ya uundaji wa sentensi changamani za Kiswahili kwa kubainisha miundo ya ndani na namna inavyopitia mageuzi hadi kupata muundo wa nje wa sentensi hizo za Kiswahili.

## 4.0 Michakato ya Uundaji wa Sentensi Changamani za Kiswahili

Data zimebainisha kuwa kuna michakato mitatu ya kisintaksia ya uundaji wa sentensi changamani za Kiswahili ambayo ni uchopekaji, udondoshaji-chopezi na udondoshaji-chopezi hamishi. Michakato hiyo imechambuliwa kama ifuatavyo:

### 4.1 Uchopekaji wa Viunganishi Tegemezi

Katika makala hii uchopekaji ni mchakato unaorejelea hali ambayo kipashio fulani ambacho hakikuwapo katika muundo wa ndani huongezwa katika muundo wa nje na kubadili hadhi ya kisintaksia ya tungo husika. Kwa mujibu wa Nadharia Rasmi uchopekaji wa vipashio ambavyo havikuwapo katika muundo wa ndani hubadili tungo fulani kutoka kuwa si bebwa (huru) kwenda kuwa bebwa (tegemezi). Imedhihirika kwamba uchopekaji hutumika kuunda sentensi changamani zenye

muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa nomino. Kishazi bebwa nomino ni kishazi ambacho hufanya kazi kama yambwa, kazi ambayo aghalabu hufanywa na kirai nomino. Hali hii hutokea mara baada ya mageuzi fulani kutokea kutoka katika muundo wa ndani kwenda muundo wa nje. Kutokana na kazi hiyo, kishazi hiki kinafahamika kama kishazi bebwa nomino. Tazama sentensi changamani ya Kiswahili yenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa nomino katika mfano wa 6(a).

6. (a) [$S_1$ Watu walisema] [$S_2$ *kwamba Wamakonde ni wacheza sindimba*] (Lema, 2004: 8).

Mfano wa 6(a) unaonesha kuwa $S_2$ ni bebwa. Hali hii ni kwa sababu tungo hiyo haiwezi kujitegemea yenyewe kimaana kutokana kuwapo kwa kiunganishi tegemezi *kwamba*. Hii ina maana kwamba katika muundo wa ndani, $S_2$ ilikuwa na hadhi sawa na $S_1$ kama inavyooneshwa katika mfano wa 6(b).

6. (b) [$S_1$Watu walisema] [$S_2$ Wamakonde ni wacheza sindimba]


Kwa kuwa kitenzi *walisema* cha $S_1$ katika 6(b) kinahitaji yambwa ili kuwa na uarifishaji kamili, palihitajika kufanyika mchakato wa kisintaksia wa kukijaliza kitenzi hicho ili kitoe taarifa kamili. Hivyo, mchakato uliofanyika ni wa kuchopeka kiunganishi tegemezi *kwamba* kwenye upande wa $S_2$ ambako kunaifanya sentensi hiyo kufanya kazi iliyopaswa kufanywa na nomino. Tazama mfano wa 6(c) unavyoonesha uchopekaji wa kiunganishi tegemezi.

6. (c) [$S_1$ Watu walisema] [$S_2$ *kwamba* Wamakonde ni wacheza sindimba]

Kutokana na uchopekaji wa kiunganishi tegemezi *kwamba* katika mfano wa 6(c) kunaifanya $S_2$ kufanya kazi kama nomino ambapo $S_2$ hubebwa kwenye kitenzi cha $S_1$. Kadhalika, baada ya uchopekaji wa kiunganishi tegemezi katika $S_{2,}$ hufanya $S_1$ na $S_2$ kuunganishwa na kuwa sentensi moja ambayo ni sentensi changamani. Kwa ufafanuzi zaidi, tazama muundo wa nje unaowasilishwa na mfano namba 6(d).

6. (d) Watu walisema *kwamba* Wamakonde ni wacheza sindimba.

Kwa hiyo, inadhihirika kwamba uchopekaji wa kiunganishi tegemezi *kwamba* katika muundo wa nje wa $S_2$ ndio unaoifanya sentensi hiyo kuwa bebwa. Hatimaye, tunapata sentensi changamani za Kiswahili zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa nomino katika muundo wa nje. Katika muundo kama huo, kishazi bebwa nomino hufanya kazi ya kujaliza kitenzi cha $S_1$ kama inavyooneshwa katika Kielelezo Na. 1.




***Kielelezo** Na. 1: Muundo wa Nje wa Sentensi Changamani ya Kiswahili Iliyoundwa kwa Uchopekaji wa Kiunganishi Tegemezi*

Kielelezo Na. 1 kinaonesha kuwa $S_2$ inafanya kazi ya kujaliza kitenzi cha $S_1$. Kazi inayofanywa na $S_1$ kwa kawaida ilipaswa kufanywa na nomino, yaani kitenzi *alisema* ni elekezi. Hivyo, kinahitaji nomino ili kutoa uarifishaji kamili. Yumkini kutokana na dhima ya kishazi bebwa nomino, ndiyo iliyomshawishi Wesana-Chomi (2017) kudai kwamba sentensi changamani zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa nomino huundwa kwa mchakato wa ujalizaji. Hata hivyo, matokeo yanaonesha kuwa ujalizaji ni tokeo la uchopekaji wa kiunganishi tegemezi katika tungo kama ilivyodhihirishwa katika mfano wa 6(c). Kwa hiyo, kisintaksia sentensi changamani za Kiswahili zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa nomino huundwa kwa mchakato wa uchopekaji wa viunganishi tegemezi kwenye $S_2$. Uchopekaji huo huifanya $S_2$ kufanya kazi ya kujaliza kiambajengo cha $S_1$, hususani kitenzi.

Pia, mchakato wa uchopekaji wa viunganishi tegemezi umedhihirika kuunda sentensi changamani za Kiswahili zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa elezi. Kishazi bebwa elezi ni kishazi ambacho hufanya kazi kama kielezi, kazi ambayo aghalabu hufanywa na kielezi au kirai kielezi. Hali hii hutokea mara baada ya mageuzi fulani kutoka katika muundo wa ndani kwenda muundo wa nje. Kutokana na kazi hiyo, kishazi hiki hufahamika kama kishazi bebwa elezi. Tofauti na uchopekaji wa viunganishi tegemezi vinavyojidhihirisha katika mfano namba 6(a-d), viunganishi tegemezi hivi huwa ni maalumu. Viunganishi tegemezi maalumu vinaweza kuwa kirai kama vile: *kwa sababu, kama vile*, na *kwa kuwa*. Pia, viunganishi hivi vinaweza kuwa kategoria ya neno kama vile *ili*, *kama na kwani*. Vilevile, viunganishi hivi vinaweza kuwa viambishi lakini bado vikafanya kazi kama kiunganishi. Viambishi vinavyoweza kutumika kama viunganishi ni vya masharti na urejeshi. Mara nyingi viunganishi tegemezi

maalumu hutangulia kishazi bebwa elezi. Tazama mfano wa 7(a) kwa ufafanuzi zaidi.

7. (a) [$S_1$ Hamiata alinuna kabisa] [$S_2$ *kwani Felisia alikuwa amemuaibisha*]
(Lema, 2004: 4)

Mfano wa 7(a) unaonesha kwamba $S_2$ haina hadhi sawa na $S_1$. Hii ni kwa sababu $S_2$ ina kiunganishi tegemezi maalumu cha sababu. Maelezo haya yana maana kwamba katika muundo wa ndani wa tungo hiyo, $S_1$ na $S_2$ zilikuwa na hadhi sawa kabla $S_2$ haijachopekwa kiunganishi hicho kama mfano wa 7(b) unavyoonesha.

7. (b) [$S_1$ Hamiata alinuna kabisa] [$S_2$ Felisia alikuwa amemuaibisha]


Mfano wa 7(b) unaonesha kuwa kitenzi cha $S_1$ kina kielezi chake ambacho ni *kabisa*. Hata hivyo, kielezi hicho kinaonekana hakielezi wazi kwa nini *Hamiata alinuna*. Hivyo, huhitajika mchakato wa kisintaksia utakaowezesha kuwapo kwa maelezo toshelevu ya sababu ya *kununa kwa Hamiata*. Kwa sababu hiyo, uchopekaji wa kiunganishi tegemezi cha sababu ya tendo, ambacho ni *kwani*, kimepachikwa mwanzoni mwa $S_2$ kama inavyojidhihirisha katika mfano wa 7(c).

7. (c) [$S_1$ Hamiata alinuna kabisa] [$S_2$ *kwani* Felisia alikuwa amemuaibisha]

Uchopekaji wa kiunganishi tegemezi cha sababu *kwani* mwanzoni mwa $S_2$ unaifanya sentensi hiyo kufanya kazi kama kielezi cha kitenzi cha $S_1$, yaani kueleza sababu ya *Hamiata kununa*. Hatua inayofuata ni kuunganisha $S_1$ na $S_2$ ili kupata muundo wa nje kama inavyooneshwa katika mfano wa 7(d).

7. (d) Hamiata alinuna kabisa *kwani* Felisia alikuwa amemuaibisha.

Mchakato wa kuchopeka kiunganishi tegemezi kabla ya $S_2$ huifanya sentensi hiyo kushuka hadhi na kufanya kazi kama kielezi. Hatimaye, tunapata sentensi changamani yenye kishazi kikuu na kishazi bebwa elezi katika muundo wa nje ambapo $S_2$ hubebwa ndani ya kitenzi cha $S_1$ kama inavyooneshwa katika Kielelezo Na. 2.




***Kielelezo Na. 2:*** *Sentensi Changamani ya Kiswahili IIiyoundwa kwa Uchopekaji wa Kiunganishi Tegemezi*

Kielelezo Na. 2 kinaonesha $S_2$ imekunjiwa ndani ya kitenzi cha $S_1$. $S_2$ katika kielelezo hicho inaonesha kuwa dhima ya sentensi hiyo ni kueleza kwa nini Hamiata alinuna. Kazi hiyo ya $S_2$ kwa kawaida ilipaswa kufanywa na kielezi. Hivyo, kwa kuwa kishazi hicho kinafanya kazi hiyo ya uelezi, ndio maana huitwa kishazi bebwa elezi, jina ambalo limetokana na dhima ya kishazi hicho.

**4.2 Udondoshaji-Chopezi**

Udondoshaji-chopezi ni miongoni mwa michakato ya uundaji wa sentensi changamani za Kiswahili uliodhihirika katika makala hii. Mchakato huo unahusu uondoaji wa kipashio radidi kinachojitokeza katika muundo wa ndani ili kuondoa uradidi huo. Kipashio kinachodondoshwa hufidiwa kwa kupachika kipashio kingine. Udondoshaji-chopezi ndio hufanya tungo zilizokuwa na hadhi sawa katika muundo wa ndani kuwa na hadhi tofauti, yaani tungo moja kubebwa ndani ya nyingine katika muundo wa nje. Imebainika kwamba mchakato huu hutumika kuunda sentensi changamani za Kiswahili zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa elezi. Pia, huundwa na sentensi changamani zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa vumishi. Mfano wa 8(a) unaonesha namna sentensi changamani za Kiswahili zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa vumishi zinavyoweza kuundwa kwa mchakato wa udondoshaji-chopezi.

8. (a) [$S_1$ Mtu mwingine tunamwita mwizi] [$S_2$ *kwa sababu tumemkamata akiiba*] (*Mwananchi*, 26. 06. 2021: 19)

Mfano wa 8(a) ni sentensi changamani yenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa elezi. $S_2$ inatoa maelezo ya kwa nini hasa mtu mwingine tunamwita *mwizi*. Hii ni kutokana na udondoshaji uliofanyika katika muundo wa ndani na kuchopekwa kirai kihusishi *kwa sababu* katika muundo wa nje, ambacho hufanya

kazi ya uunganishaji tegemezi. Hii ina maana kwamba kabla ya mchakato wa udondoshaji-chopezi, $S_1$ na $S_2$ za mfano wa 8(a) zilikuwa na hadhi sawa kama inavyooneshwa katika mfano wa 8(b).

8. (b) [$S_1$ Mtu mwingine tunamwita mwizi] [$S_2$ Tumemkamata mwizi akiiba]

Nomino *mwizi* katika mfano wa 8(b), inajitokeza katika $S_1$ na $S_2$. Ili kuondoa uradidi, nomino moja hudondoshwa kama inavyooneshwa katika mfano wa 8(c).

8. (c) [$S_1$ Mtu mwingine tunamwita mwizi] [$S_2$ tumemkamata ~~mwizi~~ akiiba]


Katika mfano wa 8(c) nomino *mwizi* ya $S_2$ imekatwa kuonesha kwamba imedondoshwa. Udondoshaji huo hufidiwa kwa kupachika kirai kihusishi kinachofanya kazi kama kiunganishi tegemezi cha sababu. Tazama uchopekaji wa kirai kihusishi *kwa sababu* katika mfano wa 8(d).

8. (d) [$S_1$ Mtu mwingine tunamwita mwizi] [$S_2$ *kwa sababu* tumemkamata akiiba]

Kutokana na upachikaji huo, $S_2$ inakuwa bebwa na kufanya kazi ya kueleza sababu ya tendo la $S_1$. Kwa hiyo, hubebwa ndani ya kitenzi cha $S_1$ kama inavyooneshwa katika mfano wa 8(e).

8. (e) Mtu mwingine tunamwita mwizi kwa sababu tumemkamata akiiba.

Mchakato huu wa udondoshaji-chopezi huifanya sentensi iliyokuwa kuu kuwa bebwa. Hatimaye, tunapata sentensi changamani yenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa elezi kama inavyooneshwa katika Kielelezo Na. 3.




*Kielelezo Na. 3: Muundo wa Nje wa Sentensi Changamani ya Kiswahili Iliyoundwa kwa Udondoshaji-Chopezi*

Kielelezo Na. 3 kinaonesha namna kirai kihusishi kinachofanya kazi ya uunganishaji tegemezi kilivyopachikwa na kuifanya $S_2$ kuwa bebwa na kufanya kazi kama kielezi. Katika kielelezo hicho, $S_2$ inaeleza kwa nini mtu mwingine anaitwa mwizi. Pia, data za utafiti zinaonesha kwamba udondoshaji-chopezi wa vipashio unatumika kuunda sentensi changamani za Kiswahili zenye muundo wa kishazi bebwa na kishazi bebwa vumishi Kishazi bebwa vumishi huitwa pia kishazi rejeshi. Mekacha (1983) anaeleza kuwa kishazi bebwa vumishi ni miongoni mwa tungo tegemezi iliyoshushwa hadhi na kutegemezwa ndani ya tungo nyingine. Anaongeza kuwa tungo tegemezi haitokei peke yake bali kama sehemu ya sentensi na kimuundo tungo tegemezi huwa kiambajengo cha sentensi nyingine. Kishazi hiki huitwa kishazi bebwa vumishi kwa sababu kinapokunjiwa ndani ya kiambajengo kingine hufanya kazi kama kivumishi. Tazama mfano wa 9(a) kwa ufafanuzi zaidi.

9. (a) [$S_1$ Baadaye walihamia chumbani] [$S_2$ *ambako mengi yalifanyika kati yao*] (*Mwananchi*, 26. 06. 2021: 20)

Katika mfano wa 9(a), $S_2$ haina hadhi sawa na $S_1$. Hii ni kutokana na udondoshaji-chopezi uliofanyika wa kiima cha $S_2$ na kufidiwa na umbo *amba* lenye kiambishi rejeshi {-ko} lililoifanya $S_2$ kuwa bebwa. Hii ina maana kwamba $S_2$ ilikuwa na hadhi sawa na $S_1$ katika muundo wa ndani kabla ya mchakato wa udondoshaji-chopezi kutokea, kama inavyooneshwa katika mfano wa 9(b).

9. (b) [$S_1$ Walihamia chumbani baadaye] [$S_2$ chumbani mengi yalifanyika kati yao]

Mfano wa 9(b) unaonesha kwamba nomino *chumbani* ya $S_1$ ndiyo hiyohiyo inayozungumziwa katika $S_2$. Hivyo, kuondoa uradidi na kuleta ushikamani katika tungo nomino moja, hususani ile ya $S_2$, hudondoshwa kama inavyoonesha hapa chini katika 9(c).

9. (c) [$S_1$ Walihamia chumbani baadaye] [$S_2$ ~~chumbani~~ mengi yalifanyika kati yao]


Nomino *chumbani* ya $S_2$ katika 9(c) imekatwa kuonesha kuwa imedondoshwa ili kuondoa uradidi. Aghalabu nomino inapodondoshwa huhitaji kipashio kingine ili kufidia pengo linaloachwa na udondoshaji huo. Kutokana na udondoshaji huo, kiambishi {-ko} hupachikwa kwenye umbo *amba* ili kufidia nomino ya $S_2$ iliyodondoshwa. Kiambishi kinachopachikwa kwenye umbo hilo hufanya kazi kama kiunganishi tegemezi. Tazama mfano wa 9(d) kwa ufafanuzi zaidi.

9. (d) [$S_1$ Baadaye walihamia chumbani] [$S_2$ *amba**ko*** mengi yalifanyika kati yao]

Mfano wa 9(d) unaonesha kuwa udondoshaji-chopezi uliofanyika katika $S_2$ umeifanya tungo hiyo kuwa bebwa kwa kuwa inafanya kazi kama kikumushi cha $KN_1$ cha $S_1$. Pia, ukichunguza kielezi *baadaye* katika mfano wa 9(d) kimehama kutoka upande wa kiarifu wa $S_1$ kama ilivyokuwa katika mfano wa 9(b) kwenda upande wa kiima cha sentensi hiyo. Kuhama huko kunakifanya kiunganishi tegemezi chenye kirejeshi *ambako* kiwe karibu kabisa na kisabiki chake (nomino inayorejelewa) ambacho ni *chumbani*. Hivyo, kutokana na mchakato huo, $S_1$ na $S_2$ huunganishwa kama inavyooneshwa katika muundo wa nje kwenye 9(e).

9. (e) Baadaye walihamia chumbani ambako mengi yalifanyika kati yao.

Katika mfano wa 9(e) udondoshaji-chopezi umeifanya $S_2$ kuwa kishazi bebwa vumishi kwa kuwa inavumisha $KN_2$ cha $S_1$. Matokeo yake ni kuundwa kwa sentensi changamani yenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa vumishi kama inavyooneshwa katika Kielelezo Na. 4




*Kielelezo Na. 4: Muundo wa Nje wa Sentensi Changamani ya Kiswahili Iliyoundwa kwa Udondoshaji-Chopezi*

Katika Kielelezo Na. 4, $S_2$ imekunjiwa ndani ya $KN_2$ cha $S_1$ kuonesha inafanya kazi ya kuvumisha kirai nomino hicho. Matokeo ya kupata sentensi changamani yenye kishazi kikuu na kishazi bebwa vumishi yanatokana na mchakato wa udondoshaji-chopezi uliotokea katika vishazi viwili ambavyo katika muundo wa ndani vilikuwa na hadhi sawa lakini baadaye kishazi kimoja kilishushwa hadhi kama ilivyoelezwa katika mfano wa 9(a-e).

Kuhusu mchakato huu wa udondoshaji-chopezi, msomaji anaweza kujiuliza, inakuwaje mchakato mmoja unazalisha miundo miwili tofauti ya sentensi changamani za Kiswahili. Sentensi hizo ni sentensi changamani zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa elezi na sentensi zenye kishazi kikuu na kishazi bebwa vumishi. Majibu yake ni kwamba sentensi changamani za Kiswahili zenye miundo hiyo huundwa kwa mchakato wa udondoshaji-chopezi, ingawa hutofautiana kwenye vipashio vinavyochopekwa baada ya udondoshaji. Kwa mfano, sentensi changamani zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa elezi huchopekwa kiunganishi tegemezi kama vile: *kwani, kwa sababu, ili* na *kwa kuwa* baada ya udondoshaji. Aidha, sentensi changamani zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa vumishi huchopekwa viambishi rejeshi vinavyopatana na nomino inayorejeshwa. Vipashio vinavyopachikwa ndivyo vinavyotofautisha miundo ya sentensi hizo changamani.

### 4.3 Udondoshaji-Chopezi Hamishi

Udondoshaji-chopezi hamishi ni miongoni mwa michakato inayotumika kuunda sentensi changamani za Kiswahili uliobainishwa katika makala hii. Udondoshaji-chopezi hamishi ni mchakato wa kudondosha kipashio kinachojirudia katika tungo na kupachika kipashio kingine cha ufidiaji, kisha kuhamisha kipashio hicho ili kuleta ushikamani katika tungo. Tazama mfano wa 10(a) kwa ufafanuzi zaidi.

10. (a) Nguo *alizovaa* zilimfanya aonekane kijana (Lema, 2004: 7).

Katika mfano wa 10(a) tungo iliyoandikwa kwa hatimlazo ni ile iliyoshushwa hadhi kutokana na mchakato wa udondoshaji-chopezi hamishi uliofanyika katika tungo. Hii ina maana kwamba tungo ya 10(a) katika muundo wa ndani, ilikuwa na vishazi viwili ambavyo vilikuwa na hadhi sawa kabla ya mchakato wa udondoshaji-chopezi hamishi kama inavyooneshwa katika 10(b).

10. (b) [$S_2$ Nguo [$S_2$ Nguo alizovaa] zilimfanya aonekane kijana].

Nomino *nguo* katika tungo ya 10(b) inajirudia kwenye $S_1$ na $S_2$. Tunasema inajirudia kwa sababu nomino *nguo* inayozungumziwa katika $S_1$ na $S_2$ ni ileile. Hivyo, udondoshaji unahitajika ili kuondoa uradidi kama mfano wa 10(c) unavyoonesha.

10. (c) [Nguo [~~nguo~~ alizovaa] zilimfanya aonekane kijana.]

Katika mfano wa 10(c), *nguo* ya $S_2$ imekatwa kuonesha kuwa imedondoshwa ili kuondoa uradidi. Hii ina maana kwamba sehemu ilipokuwapo nomino *nguo* inabaki wazi na sehemu hiyo inapaswa kuzibwa kwa kupachika kipashio kingine kitakachofidia udondoshaji huo. Kipashio hicho ni kiambishi rejeshi {-zo-} kama inavyooneshwa katika mfano wa 10(d).

10. (d) Nguo alivaa -*zo*- zilimfanya aonekane kijana.


Katika mfano wa 10(d) kiambishi rejeshi kimekaa peke yake na kipo mbali na kisabiki chake ambacho ni nomino *nguo*. Hivyo, kinahitaji kuhama na kupachikwa kwenye kitenzi kilichopo karibu na kisabiki chake kama ilivyo katika mfano wa 10(e).

10. (e) Nguo ali**zo**vaa -zo- zilimfanya aonekane kijana.

Uhamishaji wa kiambishi rejeshi katika $S_2$, huifanya sentensi hiyo kushuka hadhi na kuwa bebwa, yaani kishazi bebwa vumishi ndani ya $KN_1$ cha $S_1$. Hivi ndivyo sentensi changamani za Kiswahili zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa vumishi zinavyoundwa kama ilivyooneshwa katika muundo wa nje wa 10(f).

10. (f) Nguo alizovaa zilimfanya aonekane kijana.

Tungo ya 10(f) inaweza kufafanuliwa zaidi na Kielelezo Na. 5 kinachoonesha jinsi $S_2$ inavyofanya kazi ya kukumusha $KN_1$ cha $S_1$ kama ifuatavyo.




*Kielelezo Na. 5: Muundo wa Nje wa Sentensi Changamani ya Kiswahili Iliyoundwa kwa Udondoshaji-Chopezi Hamishi*

Kielelezo Na. 5 kinaonesha matokeo ya mchakato wa udondoshaji-chopezi hamishi ambapo mchakato huu hukifanya kishazi kikuu kimojawapo kufanya kazi kama kivumishi. Katika hicho, $S_2$ inafanya kazi kama kivumishi ambapo inavumisha $KN_1$ cha $S_1$. Pia, mfano wa 11(a) unafafanua zaidi kuhusu namna mchakato wa udondoshaji-chopezi hamishi unavyotumika kuunda sentensi changamani za Kiswahili zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa vumishi.

11. (a) Mtoto *aliyekuwa anacheza hapo nyumbani* alikwenda kumuita (Lema, 2004: 13).

Katika mfano wa 11(a), tungo iliyoandikwa kwa hatimlazo ni tungo iliyoshushwa hadhi baada ya mchakato wa udondoshaji-chopezi hamishi. Hii ina maana kwamba katika muundo wa ndani, tungo iliyoandikwa kwa hatimlazo katika 11(a) ilikuwa na hadhi sawa na hiyo ambayo haijaandikwa kwa hatimlazo kabla ya mchakato wa udondoshaji-chopezi hamishi kama inavyooneshwa katika mfano wa 11(b).

11. (b) $S_1$ Mtoto alikwenda kumuita.
$S_2$ Mtoto alikuwa anacheza hapo nyumbani.

Katika mfano wa 11(b), *mtoto* anayezungumziwa katika $S_1$ na $S_2$ ni yuleyule. Hivyo, nomino moja hudondoshwa ili kuondoa uradidi. Aghalabu nomino inayodondoshwa ni ile ya $S_2$ kama inavyooneshwa katika mfano wa 11(c).

11. (c) Mtoto [~~mtoto~~ alikuwa anacheza hapo nyumbani] alikwenda kumuita.

Nomino radidi *mtoto* ya $S_2$ katika 11(c) imekatwa kuonesha kuwa imedondoshwa. Udondoshaji huu hufanyika ili kuondoa uradidi na kuleta ushikamani katika tungo husika. Kutokana na udondoshaji wa nomino radidi katika $S_2$ mahali nomino hiyo ilipokuwa panabaki wazi kama inavyooneshwa katika mfano wa 11(d).

11. (d) Mtoto [……..alikuwa anacheza hapo nyumbani] alikwenda kumuita.

Katika mfano wa 11(d) panahitajika kupachikwa kipashio kingine ambacho kitaziba pengo hilo. Katika mazingira kama haya, kiambishi rejeshi ndicho hupachikwa ili kuziba pengo la nomino iliyodondoshwa kama inavyooneshwa hapa chini katika mfano wa 11(e).

11. (e) Mtoto [-ye- alikuwa anacheza hapo nyumbani] alikwenda kumuita.


Katika mfano wa 11(e) inaonesha kiambishi {-ye-} kipo peke yake ilhali kwa kawaida katika Kiswahili kiambishi rejeshi huchopekwa kwenye kitenzi kikuu, kisaidizi au kwenye umbo maalumu AMBA. Hivyo, kiambishi hicho huhitajika kuhama ili kipachikwe ndani ya kitenzi kilicho karibu na kisabiki chake. Tazama mfano wa 11(f) kwa ufafanuzi zaidi.

11. (f) Mtoto [ ~~ye~~ ali**ye**kuwa anacheza hapo nyumbani] alikwenda kumuita.

Baada ya uhamishaji wa kiambishi rejeshi kutoka mahali kilipokuwa na kupachikwa kwenye kitenzi, hukifanya kitenzi cha kishazi hicho kuwa bebwa. Uhamishaji huo ndio unaokamilisha sentensi changamani ya Kiswahili yenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa vumishi kama inavyooneshwa katika muundo wa nje kwenye mfano wa 11(g).

11. (g) Mtoto aliyekuwa anacheza hapo nyumbani alikwenda kumuita.

Tungo ambayo huwa na kiambishi rejeshi ndiyo huitwa kishazi bebwa vumishi. Kishazi hiki aghalabu hufanya kazi ya kukumusha KN kama inavyooneshwa kwenye Kielelezo Na. 6.




*Kielelezo Na. 6: Sentensi Changamani ya Kiswahili Iliyoundwa kwa Udondoshaji-Chopezi Hamishi*

Kielelezo Na. 6 kinaonesha matokeo ya mchakato wa udondoshaji-chopezi hamishi ambapo mchakato huu hukifanya kishazi kikuu kimojawapo kufanya kazi kama kivumishi. Katika hicho, $S_2$ inafanya kazi kama kivumishi ambapo inavumisha $KN_1$ cha $S_1$. Mchakato wa udondoshaji-chopezi hamishi ambao Wesana-Chomi (2017) ameuita mchakato wa urejeshaji umebainisha jinsi unavyounda sentensi changamani za Kiswahili zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa vumishi. Kwa hakika, kuuita mchakato huu urejeshaji hasa kwa kuwa nomino radidi inageuzwa na kuwa kirejeshi, kunasailika (rej. mfano namba 10 na 11 kwa ufafanuzi zaidi). Hii ni kwa sababu, kisintaksia nomino radidi hudondoshwa ili kuondoa uradidi na kuleta ushikamani katika tungo. Baada ya udondoshaji huo, uchopekaji hufanyika ili kufidia kipashio kilichodondoshwa. Kipashio hicho huwa ni kiambishi rejeshi. Ikiwa kiambishi hicho kipo mbali na kisabiki chake, huhamishwa ili kiwe karibu na kisabiki au kirejelewa chake. Maelezo kutoka mfano wa 10 na 11 yanadhihirisha kwamba mchakato unaotumika kuunda sentensi changamani za Kiswahili zenye kishazi kikuu na kishazi bebwa vumishi ni udondoshaji-chopezi hamishi na si urejeshaji kama ilivyokuwa ikielezwa na Wesana-Chomi (2017).

**5.0 Hitimisho**

Makala hii imechambua michakato ya kisintaksia ya uundaji wa sentensi changamani za Kiswahili kwa kubainisha namna kishazi kikuu na kishazi bebwa vinavyowekwa pamoja kuunda sentensi changamani. Matokeo yanaonesha kwamba sentensi changamani huundwa kwa michakato mitatu ambayo ni uchopekaji, udondoshaji-chopezi na udondoshaji-chopezi hamishi. Kwa upande wa mchakato wa uchopekaji, imedhihirika kwamba uchopekaji hutumika kuunda sentensi changamani zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa nomino na kishazi kikuu na kishazi bebwa elezi. Hata hivyo, uchopekaji wa viunganishi tegemezi vinavyounda sentensi changamani za Kiswahili zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa nomino na kishazi kikuu na kishazi bebwa elezi ni tofauti. Utofauti huo unatokana na aina ya viunganishi tegemezi vinavyochopekwa mwanzoni mwa $S_2$. Katika muundo wa sentensi changamani zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa nomino, viunganishi tegemezi ambavyo huchopekwa ni *kuwa, kama* na *kwamba.* Kwa upande wa sentensi changamani zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa elezi, huchopekwa viunganishi tegemezi maalumu ambavyo vinaweza kuwa neno, kirai au kiambishi ambavyo hufanya kazi kama viunganishi. Aidha, kuhusu mchakato wa udondoshaji-chopezi, imebainika kwamba mchakato huu hutumika kuunda sentensi changamani zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa nomino na kishazi kikuu na kishazi bebwa elezi. Hata hivyo, imebainika kwamba kinachosababisha sentensi changamani zinaoundwa kwa mchakato mmoja kuwa na miundo tofauti ni aina ya vipashio vinavyochopekwa mara baada ya udondoshaji. Vilevile, kwa upande wa mchakato wa udondoshaji-chopezi hamishi, imebainika kwamba hutumika kuunda sentensi changamani zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa vumishi pekee. Kulingana na uchambuzi wa sentensi changamani uliofanywa katika makala kwa kutumia Nadharia Rasmi, ni dhahiri kuwa madai ya Wesana-Chomi (2017) kwamba sentensi changamani zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa nomino zinaundwa kwa mchakato wa ujalizaji kisintaksia yanasailika. Hii ni kwa sababu imebainika kuwa sentensi changamani zenye muundo huo huundwa kwa mchakato wa uchopekaji wa viunganishi tegemezi ambapo baada ya uchopekaji huo ndipo $S_2$ hufanya kazi kama kijalizo. Aidha, madai kwamba sentensi changamani zenye muundo wa kishazi kikuu na kishazi bebwa vumishi kwamba zinaundwa kwa mchakato wa urejeshaji, yamebainika kuwa na walakini. Madai yake ni kwamba nomino radidi ya $S_1$ na $S_2$ hugeuzwa na kuwa kiambishi rejeshi. Kwa mujibu wa data, imebainika kuwa nomino radidi haigeuzwi kuwa kirejeshi bali hudondoshwa ili kuondoa uradidi. Baada ya udondoshaji huo, kiambishi rejeshi hupachikwa ili kuziba pengo lililoachwa kwa udondoshaji huo. Kiambishi hicho hulazimika kuhama ili kuwa karibu na kisabiki chake. Baada ya mchakato huo, sentensi iliyopachikwa kiambishi rejeshi hufanya kazi ya kukumusha kirai nomino kinachorejeshwa.

## Marejeleo

Chomsky, N. (1965). *Aspects of the Theory of Syntax*. Cambridge: Mass MIT Press.

Kortmann, B. (1997). *Adverbial Subordination. A Typologyn and History of Adverbial Subordinators Based on European Languages*. New York: Mourton da Gruyter.

Kyungu, S.M. (2022). Uchambuzi wa Michakato ya Kisintaksia katika Uundaji wa Sentensi Changamani za Kiswahili. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Lema, E. (2004). *Mwendo*. Dar es Salaam: E&D Publishers.

Mekacha, R.D. (1987). “Tungo Rejeshi katika Kiswahili”. *Mulika*. 19: 83-91.

Meyer, C. (1996). “Coordinate Structures in English”. *World Englishes*. 15: 11-27.

Philipo, Z.T. na Kuyenga, F.E. (2017). *Sintaksia ya Kiswahili: Nadharia ya Kisintaksia na Uchanganuzi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: Karljamer Publishers Limited.

Tallerman, M. (2011). *Understanding Syntax*. London: Hodder Arnold.

Wamitila, K.W. (2016). *Kamusi Pevu ya Kiswahili*. Nairobi: Vide~Muwa.

Wesana-Chomi, E. (2017). *Kitangulizi cha Muundo Viambajengo wa Sentensi za Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

**Vifupisho Vilivyotumika:**

| | | |
|---|---|---|
| S | = | sentensi |
| KN | = | kirai nomino |
| KT | = | kirai kitenzi |
| KV | = | kirai kivumishi |
| KE | = | kirai kielezi |
| KH | = | kirai kihusishi |
| N | = | nomino |
| T | = | kitenzi |
| V | = | kivumishi |
| E | = | kielezi |
| H | = | kihusishi |
| UT | = | kiunganishi tegemezi |
| Ts | = | kitenzi kisaidizi |
| w | = | kiwakilishi |